COUNTY MOCK EXAMS-STD 8
2016

KISWAHILI PAPER

Coordinated by KENPRO,
Macjo Arcade, 4th Floor, Suite 15E,
Off Magadi Road, Ongata Rongai |Tel: +254202319748 |
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website:www.schoolsnetkenya.com

KIRINYAGA COUNTY MOCK

DARASA LA NANE - MWAKA 2016

Muda: Saa 1 Dakika 40

SEHEMU YA KWANZA:
KISWAHILI: LUGHA

SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina Maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika KARATASI YA MAJIBU na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu.

NAMBA YAKO YA MTIHANI
JINA LAKO
JINA LA SHULE YAKO

6. Kwa kuchora kistari katika kisanduku zenye namba zinazokuhusu. Onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
9. Kila swali 1 - 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa Herufi. A. B. C. D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

Kwa mfano:

Katika kijitabu cha maswali

Kamilish Methali:-
24. Mkono mmoja_____.
A. hakivunji chawa
B. hufa maskini
C. heri kuwa naye
D. hauchinji ng'ombe

Jibu sahihi ni B (Shimo)
Katika karatasi ya majibu:

23. [A] [B] [C] [D] 24. ~~[A]~~ [B] [C] [D] 25. [A] [B] [C] [D] 26. [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 30, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne uliyopewa.

FUNGUA UKURASA

Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 - 15 kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi ya yale ulivopewa

____1____ la wataalamu wa Kiswahili ____2____ ____3____ muhimu nchini. Wanasema ____4____ ikiwa zaidi ya asilimi sabini ya ____5____ wanaelew na kuzungumza Kiswahili. ____6____ haja ya kufanya ____7____ ya urais kutumia lugha ya Kiingereza. ____8____ katiba inasema lugha rasmi ____9____ Keny ni Kiswahili na Kiingereza. kumekuwa n hali ____10____ watu huona haya kujieleza kwa Kiswahili wanapokuwa ____11____ majukwaa ya ____12____.

Kiswahili si lugha ya watu walio nyuma kimaendeleo. Ni lugha yetu ambayo ____13____ ya watu kutoka mataifa ya ng'ambo wanaisoma kwa bidii kwa kuelewa umuhimu wake katika mawasiliano na pia kwa ajili ya uchumi. Vyombo vya habari vinapopanga hali ya ____14____ havina budi kuelewa wanaolengwa kufahamu ____15____ ya wanaotaka urais ni raia wa Kenya na wala si wageni wanaozungumza Kiingereza.

1.	A. Kundi	B. Kongamano	C. Rubaa	D. Tume
2.	A. imeibua	B. limeibua	C. imeimbua	D. limeubua
3.	A. suala	B. swala	C. swara	D. masuala
4.	A. kwani	B. wao	C. kwamba	D. ili
5.	A. Jamii	B. Wakenya	C. Wnanchi	D. Aila
6.	A. hakuna	B. bila	C. kuna	D. bila
7.	A. mijiadara	B. mjadala	C. mazungumzo	D. mijadala
8.	A. Madhali	B. Ingawa	C. Isipokuwa	D. Kwa vile
9.	A. za	B. ya	C. kwa	D. la
10.	A. ambazo	B. ambavyo	C. ambapo	D. ambamo
11.	A. katika	B. kwenye	C. palipo	D. ndani ya
12.	. unma	B. waatu	C. uma	D. wengi
13.	A. mamilioni	B. jopo	C. mamillioni	D. sote
14.	A. moja joja	B. moja kwa moja	C. kenyekenye	D. kwenye
15.	A. kauli	B. maoni	C. mawazo	D. sera

Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu sahihi

16. Hizi ni baadhi ya hali za kunyambua vitenzi
(i) fanyafanya (ii) Fanyua
(iii) Faanyiwa (iv) Fanyisha
Zipi zipo katika kauli ya kuradidi na amri ntawalia
A. iv, ii B. i, iii, C. i, iv D. ii, i

17. Vikembe pia ni watoto wa viumbe mbalimbali.Kisawe mwafaka pia ni
A. Visalia B. vizawe
C. Vizaliwa D. Vizaliwe

18. Makao ya ngombe ni zizi kama vile ya kipepeo ni ___
A. sega B. kichunguu
C. kifukofuko D. kidurusi

19. Andika kinyume cha sentensi ifuatayo
Koo amenunuliwa
A. Pora ameuzwa B. Tembe ameuzwa
C. Kuku ameuzwa D. Kikwara ameuzwa

20. Baada ya daktri kugundua ugonjwa wa kisukari alimshauri mgonjwa _____
A. kuzia B. kusia
C. kusiha D. kuzila

21. Shairi lenye mishororo mitano katika kila ubeti huitwa
A. tathlitha B. tarbia
C. takhmisa D. kwamba

22. Andika sentensi ifuatayo kwa wingi
Seremala ameuza hema
A. Seremala wameuza hema
B. Maseremala wameyauza hema
C. Maseremala wameuza mahema
D. Seremala wameuza mahema

23. Yesu alizaliwa katika umbo lipi kati ya haya?
A. Hiram B. Hori
C. Tiara D. Sayari

24. Ndipo moto uwake barabara mtu _____
A. huvuvua B. hufufia C. huvuvia D. hufifia

25. Onyesha sentensi yenye "na" ya hali isiyodhirika
A. Sote natuimbe wimbo wa taifa
B. Yule analiosha gari lake
C. Mwimbaji hodari anasauti ya nanga
D. Nadurusu kwa lengo la kufudafu

26. Chagua kivumishi katika sentensi ifuatayo
Mikeka michache imenunuliwa leo
A. Mikeka B. Leo
C. Michache D. Imenunuliwaa

27. **Chagua usemi wa taarifa wa**:-
"Viwekeni vyumba vyenu safi," Mama akashauri
A. Mama aliwashauri waviweke nyumba vyenu safi
B. Mama alitushauri tuviweke vyumba vyetu safi
C. Mama alimshauri mviweke vyumba vyenu safi
D. Mama alishauri viwekeni vyumba vyenu safi

28. Mwenye kukifahamu kitu ni yule ambaye kitu hicho ni chake. Ni methali ipi inalingana na maelezo haya?
A. Ganda la muwa la jana chungu kaona kivuno
B. Uchungu wa mwana aujuaye ni mzazi
C. Dau la mnyonge haliendi joshi
D. Bura yangu sibadili na rehani

29. Yupi kati ya hawa si mtoto wa nyanya?
A. Shangazi B. Ami
C. Halati D. Mpwa

30. Ni neno lipi kati ya haya halina maana ya 'mbango?'
A. Mali B. Fedha
C. Ngiri D. Pambo

Soma ufahamu ufuatao kisha ujibu maswali 31-40

Uamuzi uliofanywa na serikali wakuhimiza watoto wote warudi shuleni ni jambo mwafaka. Watoto walifurika shuleni ili kusajiliwa. Waliokuwa wakirandaranda mitaani walifuatilizwa hima hima na kupelekwa shuleni. Waliokuwa wakubwa kiumri walipelekwa kwenye shule za kiufundi. Wakatabasamu kwa furaha kama mzazi aliyepata salama.

Kwa miaka mingi baadhi ya wazazi wameshindwa kuwasomesha wanao. Hii ni kutokana na umaskini uliokithiri mipaka. Hali hiyo ilichangia huzuni miongoni mwa familia fukara. Pengo la waliosoma na likazidi kuwa pana kielimu na kiuchumi. Uadui ukaingilia jamii. Ujambazi ukajitafutia nafasi.

Sasa watu wote wkipewa haki sawa na kusoma, hata wale watoto wa walalahoi watamanio masomo watakinaisha kiu chao. Pia mengi ya matatizo yatapungua. Si kweli kuwa tajiri ni mwerevu kuliko mkata. Kila mwanajamii akipew nafasi asome kwa bidii atafua dafu maishani.

Vijana watakaofuzu katika shule za kiufundi wataweza kupata ajira katika sekta mbalimbali. Mwishowe wakipata mtaji watajiendeleza kwa kuanzisha miradi midogo midogo ya kujitegemea. Hali kama hii ikienea kote nchini viwanda vidogo vidogo vitaanzishwa na ajira kupatikana. Hiyo itakuwa njia moja wapo kuu ya kuinua uchumi na kuzalisha nafasi nyingi za kazi. Kitaluma, hawa vijana waataweza kwa madaktari, walimu na wahasibu Kisomo ni kitamu, hakifai kutiliwa nanga.

31. Maamuzi yaliyofanywa na serikali _____
A. yalisabbisha kufurika kwa watoto shuleni na kupita mitihani
B. Yalisababisha kuchipuka kwa vyuo mhusisi vy kuondoa umaskini
C. Yalikisababisha kuongezeka kw watoto shuleni na kupata nafasi ya kujiendeleza
D. Yalisababisha kupungua kwa umaskini n kuwapa watoto nafasi ya kujiendeleza

32. Maana ya kusajiliwa ni _____
A. kuandikishwa
B. kurekebishwa
C. kufundishwa
D. kunufaishwa

33. "..... baadhi ya wazazi wameshindwa kuwasomesha wanao" Chagua methali inayoafikia maelezo hayo
A. Maskini kiokota kaambiwa kaiba
B. Dau la mnyonge haliendi joshi
C. Maskini halali mchana
D. Ng'ombe wa maskini hazai pacha

34. Mali inayotumika kuanzisha au kupanulia biashara huitwaa mtaji au_____
A. akiba B. duhuli
C. hazina D. amali

35. Vijana wote wakipata mtaji _____
A. watakitilia kisomo chao maanani
B. wataanzisha shughuli za kujikimu
C. wataanzisha miradi ya kiufundi
D. watoto wa maskini watakuwa werevu

36. "..... watakinaisha kiu chao." Hii ina maana kuwa
A. watapunguza tamaa yao
B. wataitosheleza hamu yao
C. watafurahia hali yao
D. watajikimu milele

37. Kisomo hakifai kutiliwa nanga kwa sababu_____
A. kina faida nyingi
B. watu watakuwa wataalamu
C. shule zitaongezeka
D. serikali ina uwezo wa kufunza bure

38. Fua dafu ni fani gani ya lugha?
A. Msemo
B. Tashbihi
C. Methali
D. Isitiara

39. Ukosefu wa elimu husababisha _____
A. ukosefu wa kazi, utajiri na huzuni
B. wivu, tamaa, uadui na ujambazi
C. umaskini, uadui na ujambazi
D. wivu, njaa, umaskini na wizi

40. Wasio na elimu huwa maskini, fukara, walalahoi, wakata au _____
A. wazimu
B. walaheri
C. hawinde
D. wakwasi

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41-50

Ni jambo lisilopingika kuwa, elimu ni ufunguo wa maisha. Aidha elimu ni nguzo imara ya kutegemea. Hata hivyo yafaa ifahamike kuwa elimu itamfaidi mmiliki wayo yule ambaye ataitumia kwa nidhamu, hekima na heshima.

Haijalishi iwapo mahuluki ameyasoma matopa ya vitabu, amefikia kiwango kipi au anazo shahada ngapi? Iwapo hana adabu, heshima, nidhamu n uajibikaji, elimu yako haijakamilika. Elimu hiyo si lolote si chochote. Elimu yake itakuwa kama pambo wala si jebasi. Pambo haliwezi kusitiri mtu. Hiyo ni gange ya lebasi.

Ni fedheha na izara kuwaona baadhi ya insi wakichawiza kuwa wameelimika ilhali wanazo fuska. Heshima kwao ni mwiko. Adabu kwao ni msemo. Ukweli ni kuwa elimu hiyo yao haina faida kwa walimwengu. Mdarisi wangu wa zamani alinieleza kuwa kumiliki elimu ya aina hiyo ni sawa na kufunga tai huku mtu akiwa na suti ya Mungu.

Ni jambo aula mja kuonyesha elimu yake kwa vitendo. Vitendo vya aliyesoma vinafaa kupigiwa mfano. Aidha ifahamike kwamba elimu si ya vitabu tu. Lahaula! Ipo elimu ya dunia. Shari elimu yetu ituwezeshe kutafakari ya ulimwengu.

41. Kisawe cha neno lebasi ni _____
A. akili B. pambo
C. elimu D. nguo

42. Elimu mwafaka ni ipi?
A. Yenye uajibikaji
B. Ya shahada
C. Ya chekechea D. Ya sekondari

43. Adinasi hutajika ameelimik ikiwa _____
A. amesoma matopa ya vitabu
B. ana ustarabu
C. ana shahada nyingi
D. anaelewea kimombo

44. Ni nani wa maana zaidi?
A. Yeyote aliye na elimu
B. Msaliti
C. Mwenye matendo mema
D. Nduma kuwili

45. Kusudi kuu la elimu ni _____
A. kuwajibika B. kusifika kwa mmiliki
C. kufanya kazi D. kutajirika

46. Mwandishi ametaja aina ngapi za elimu?
A. Tano B. Nne
C. Kadhaa D. Mbili

47. "Ni jambo aula ....." inamaanisha
A. Ni muhali B. Si sawa
C. Ni sawa D. Ni adimu

48. Nini maana ya "akiwa na suti ya Mungu?"
A. Akiwa uchi wa mnyama
B. Akiwa zini
C. Akiwa hali mahututi
D. Akiwa mwendawazimu

49. Neno mwiko lina maana ipi katika taarifa hii?
A. Kifaa cha kusonga ugali
B. Tamaa
C. Jambo halali
D. Jambo haramu

50. Kichwa mwafaka kwa kifungu hiki ni
A. Masomo duni
B. Elimu ya ughaibuni
C. Elimu mwafaka
D. Wasomi